

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



04 FEBRUARI, 2022



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA SITA

KIKAO CHA NNE – TAREHE 04 FEBRUARI, 2022

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

26. MHESHIMIWA ALI HASSAN KING  
(JANG'OMBE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni lini Serikali itawatambua Watoto wenyewe ulemavu ambao wanaishi katika mazingira magumu ili kuwasaidia kwa matibabu na kimaisha.

27. MHESHIMIWA ALI JUMA MOHAMED  
(SHAURIMOYO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatafutia ajira na fursa mbalimbali Vijana nje ya nchi.

## **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

### **28. MHESHIMIWA ELIBARIKI IMMANUEL KINGU (SINGIDA MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia maboma ya Zahanati za Ufana, Kinyampembe, Mpetu, Misake, Mlandala, Kaugeri na Mtavira ambayo yamejengwa kwa nguvu za Wananchi kwa zaidi ya miaka mitano sasa katika Jimbo la Singida Magharibi.

### **29. MHESHIMIWA SALMA RASHID KIKWETE (MCHINGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Tamisemi):-


Je, ni lini Serikali itajenga kivuko kutoka Mchinga Moja kwenda Mchinga Mbili ili kurahisisha huduma kwa Wananchi pamoja na Wanafunzi wanaovuka Bahari kwenda Shule ya Sekondari Mchinga.

## **OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

### **30. MHESHIMIWA BONNAH LADISLAUS KAMOLI (SEGEREA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali imejipangaje kutoa elimu ya utunzaji mazingira kwa Wakulima wa Mbogamboga ikiwemo pamoja na hatua za kuchukua ili kulinda mazingira katika Bonde la Mto Msimbazi.



### **WIZARA YA MAJI:**

### **31. MHESHIMIWA MOSHI SELEMANI KAKOSO (MPANDA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya ujenzi wa mradi mkubwa wa maji toka Ziwa Tanganyika kwenda Mpanda Mjini ili kutatua tatizo la maji.

**32. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

- (a) Je, ni lini Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria Wilayani Urambo utaanza ili kutatua tatizo la Maji katika Wilaya hiyo;
- (b) Je, ni lini Serikali itachimba Mabwawa katika Kata za Iyombo na Kalamela hasa ikizingatiwa kuwa maombi yalishawasilishwa.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**33. MHESHIMIWA MARTHA FESTO MARIKI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara za kuunganisha Mkoa wa Katavi na Mikoa ya jirani utaanza.

## **WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

### **34. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliiano na Teknolojia ya Habari:-

- (a) Je, ni lini Serikali itafanya maboresho ya Mawasiliiano ya Simu katika Jimbo la Tabora Mjini hususan kwenye Kata za pembezoni;
- (b) Je, ni lini Serikali itapeleka Minara ili kuondoa changamoto hii hasa katika Kata ya Itetemla ambayo ina changamoto kubwa ya Mawasiliiano.

## **WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

### **35. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

- (a) Je, ni lini Mikataba ya miradi mbalimbali ya migodi ya Madini, ujenzi wa Bandari Bagamoyo, ujenzi wa Reli (SGR), ujenzi

wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, bomba la mafuta na mradi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam italetwa Bungeni ili kupata ufahamu wa miradi hiyo;

- (b) Je, katika Mikataba hii ni mingapi imewahi kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**36. MHESHIMIWA ASIA ABDULKARIMU HALAMGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Wakandarasi wa Tanzania wanapata fursa ya kujenga mnara wa Mwalimu Nyerere katika Makao Makuu ya Umoja wa Afrika hasa ikizingatiwa Serikali ya Tanzania ndio inasimamia ujenzi wa mnara huo.

## **WIZARA YA AFYA:**

### **37. MHESHIMIWA ESTHER LUKAGO MIDIMU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, ni lini Serikali itatoa kibali kuruhusu ujenzi wa Kiwanda cha kuzalisha Vifaa Tiba vitokanavyo na malighafi ya pamba; kwa kuwa utaratibu wa kuanza ujenzi umeshakamiliaka lakini kibali cha Ujenzi toka Serikali kuu kimechukua muda mrefu.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **38. MHESHIMIWA VITA RASHID KAWAWA (NAMTUMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurudisha silaha kwa wamiliki halali ambazo zilichukuliwa na Serikali wakati wa zoezi la Operesheni Tokomeza.

### **39. MHESHIMIWA OMAR ALI OMAR (WETE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati jengo kongwe la Polisi Wete ambalo lipo katika hali mbaya;
- (b) Je, ni lini Serikali itayatengeneza magari ya Polisi Mkoa wa Kaskazini Pembra ambapo kwa sasa ni gari moja tu linafanya kazi.

**DODOMA  
04 FEBRUARI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**